

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
TAASISI YA ELIMU TANZANIA**



**MUHTASARI WA SOMO LA UPIMAJI NA AFUA STAHIKI KWA MWALIMU
TARAJALI WA FANI YA ULEMAVU WA AKILI NA USONJI
ASTASHAHADA YA UALIMU ELIMU MAALUMU**

© Taasisi ya Elimu Tanzania, 2019

Toleo la Kwanza 2019

ISBN: 978-9976-61-855-6

Taasisi ya Elimu Tanzania

S.L.P. 35094

Dar es Salaam

Tanzania

Simu: +255 222 773 005

Faksi: +255 222 774 420

Baruapepe: director.general@tie.go.tz

Tovuti: www.tie.go.tz

Muhtasari huu urejelewe kama: Taasisi ya Elimu Tanzania. (2019). Muhtasari wa Somo la Upimaji na Afua Stahiki kwa Mwalimu Tarajali Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu. Dar es Salaam: Taasisi ya Elimu Tanzania.

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kurudufu, kuchapisha, kutafsiri wala kuutoa muhtasari huu kwa namna yoyote ile bila idhini ya maandishi kutoka Taasisi ya Elimu Tanzania.

Idhini

Mafunzo ya Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu ni ya miaka miwili na yamekusudiwa kumuandaa mwalimu tarajali kuwa mahiri na mwenye uwezo wa kufanya kazi kwa dhati na kwa weledi. Mwalimu huyo atafundisha katika shule za msingi zinazodahili wanafunzi wenye mahitaji maalumu. Mwalimu tarajali atatambuliwa kuwa ni mwalimu baada ya kuhitimu mafunzo ya Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu na kufaulu mafunzo ya nadharia na mafunzo ya ualimu kwa vitendo.

Muhtasari huu umeidhinishwa kuwa ni wa somo la Upimaji na Afua Stahiki kwa mwalimu tarajali wa fani ya ulemavu wa akili na usonji katika Mafunzo ya Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu.



Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa
Kaimu Kamishna wa Elimu
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia
S.L.P. 10
Dodoma

Simu: +255 262 963 533
Baruapepe: info@moe.go.tz
Tovuti: www.moe.go.tz

YALIYOMO

Idhini	iii
1.0 Taarifa za Awali	1
1.1 Utangulizi	1
1.2 Muundo wa Muhtasari	1
1.3 Sababu za Kuandaa Muhtasari	2
1.4 Malengo ya Elimu Nchini Tanzania	2
1.5 Malengo ya Jumla ya Mafunzo ya Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu	3
1.6 Madhumuni ya Mafunzo ya Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu	3
1.7 Umahiri wa Jumla wa Mafunzo ya Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu	4
1.8 Malengo ya Somo la Upimaji na Afua Stahiki	5
1.9 Upimaji na Tathmini	6
1.10 Muda wa Mafunzo	7
1.11 Maudhui ya Muhtasari wa Somo	7
2.0 Maudhui ya Muhtasari	8
2.1 Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi wa Somo	8
2.2 Maudhui ya Ufundishaji wa Somo	10

Majedwali

Jedwali namba 1: Upimaji Endelevu na Upimaji Tamati	6
Jedwali namba 2: Umahiri wa Somo la Upimaji na Afua Stahiki kwa Mwalimu Tarajali wa Fani ya Ulemavu wa Akili na Usonji	8
Jedwali namba 3: Maudhui ya Ufundishaji wa Somo la Upimaji na Afua Stahiki kwa Mwalimu Tarajali wa Fani ya Ulemavu wa Akili na Usonji	10
Orodha ya Machapisho	31

1.0 Taarifa za Awali

1.1 Utangulizi

Muhtasari huu wa somo la Upimaji na Afua Stahiki umeandaliwa kutokana na Mtaala wa Mafunzo ya Ualimu Elimu Maalumu wa mwaka 2019. Muhtasari huu unalenga kumjengea mwalimu tarajali maarifa, stadi na mwelekeo utakaomwezesha kukabiliana na mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji wa mwanafunzi mwenye ulemavu wa akili na mwanafunzi mwenye usonji aliyedahiliwa katika elimu ya msingi.

Ili kumsaidia mkufunzi, yametolewa mapendekezo ya mbinu za kufundishia na kujifunzia, zana/vifaa vya kufundishia na kujifunzia pamoja na upimaji. Mkufunzi anahimizwa kutumia mbinu mbalimbali na zana zinazopatikana kwenye mazingira yanayohusika na upimaji ulioshauriwa kwenye muhtasari huu. Pamoja na mbinu zilizoainishwa kwenye muhtasari huu mkufunzi anaweza kutumia mbinu nyingine tofautitofauti kulingana na mazingira na mahitaji ya mwalimu tarajali na umahiri unaojengwa.

1.2 Muundo wa Muhtasari

Muhtasari huu umegawanyika katika sehemu kuu mbili. Sehemu ya kwanza ina taarifa za awali na sehemu ya pili ni maudhui ya muhtasari.

Sehemu ya kwanza inajumuisha utangulizi, muundo wa muhtasari, sababu za kuandaa muhtasari, malengo ya elimu nchini Tanzania, malengo ya jumla ya mafunzo ya astashahada ya ualimu elimu maalumu, madhumuni ya mafunzo ya astashahada ya ualimu elimu maalumu, umahiri wa jumla wa mafunzo ya astashahada ya ualimu elimu maalumu, malengo ya somo la Upimaji na Afua Stahiki, upimaji na tathmini na muda wa mafunzo. Sehemu ya pili inajumuisha maudhui ya muhtasari wa somo.

1.3 Sababu za Kuandaa Muhtasari

Dira ya elimu na mafunzo inasisitiza kuwapo kwa mwalimu aliye bora kitaaluma na kitaalamu na mwenye mbinu mbalimbali za kujifunzia na kufundishia somo la Upimaji na Afua Stahiki ili kukabiliana na changamoto za mahitaji na matarajio ya kielimu kulingana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia.

Mwelekeo wa dira na mpango wa elimu kwa ujumla ni kumwandaa mwalimu mwenye ujuzi wa kumfundisha mwanafunzi mwenye ulemavu wa akili na mwenye usonji katika shule za msingi kwa kuzingatia misingi, kanuni na mielekeo inayopasa. Mwalimu tarajali wa somo la Upimaji na Afua Stahiki kwa ajili ya mwanafunzi mwenye ulemavu wa akili na mwanafunzi mwenye usonji anahitaji kupata ujuzi wa kuweza kuyatumia vema mazingira yake.

1.4 Malengo ya Elimu Nchini Tanzania

Elimu inayotolewa ni ya kurithisha maarifa, stadi na mielekeo bora kutoka kwa vizazi vilivyopita hadi vizazi vya wakati huu na vijavyo. Hivyo, yafuatayo ndiyo malengo makuu ya elimu nchini:

- a) kuendeleza na kukuza maendeleo, kuboresha haiba ya wananchi wa Tanzania, rasilimali zao na matumizi bora ya rasilimali hizo katika kuleta maendeleo ya mtu binafsi na ya kitaifa;
- b) kukuza tabia ya kuthamini utamaduni, mila na desturi za watanzania;
- c) kukuza upatikanaji wa fursa za kusoma, kuandika na kuhesabu na matumizi sahihi ya maarifa na stadi za kijamii, kisayansi, kiufundi, kiteknolojia, kitaalamu na aina nyingine za maarifa na ujuzi, kwa ajili ya maendeleo na kuboresha hali ya mtu na jamii;
- d) kukuza na kuendeleza kujiamini, kudadisi, weledi na kuheshimu utu wa mtu na haki za binadamu na kuwa tayari kufanya kazi kwa kujiendeleza na kwa maendeleo ya Taifa;
- e) kuwezesha na kupanua mawanda ya kujipatia maarifa, kuboresha na kukuza stadi za kiakili, utendaji, uzalishaji na nyingine zinazotakiwa katika kukidhi mabadiliko ya mahitaji kiuchumi;

- f) kumwezesha kila raia kuelewa misingi ya katiba ya nchi pamoja na kuthamini haki za binadamu na uraia, wajibu na majukumu yanayoendana nayo;
- g) kukuza utashi wa kupenda na kuheshimu kazi za kujiajiri na kuajiriwa na kuboresha utendaji kazi katika sekta za uzalishaji na huduma;
- h) kujenga misingi ya maadili yanayokubalika kitaifa na ushirikiano wa kitaifa na kimataifa, amani na sheria kwa njia ya kujifunza;
- i) kuwezesha kuwapo kwa matumizi sahihi, usimamizi na utunzaji wa mazingira; na
- j) kujenga tabia na utamaduni wa kuwakubali watu wenye ulemavu na kuwashirikisha kwenye nyanja zote za maisha kwa maendeleo ya Taifa.

1.5 Malengo ya Jumla ya Mafunzo ya Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu

Mafunzo ya Ualimu Elimu Maalumu yatamsaidia kujenga umahiri kwa mwalimu tarajali katika:

- a) nadharia za saikolojia ya elimu, malezi, ushauri na huduma kwa watu wenye mahitaji maalumu;
- b) kugundua na kubuni mbinu na njia za kufundishia na kujifunzia;
- c) uchambuzi wa mtaala na vifaa vya mtaala;
- d) kumudu stadi kuu za masomo ya lugha, sanaa na maendeleo ya sayansi na teknolojia;
- e) kufanya upimaji na tathmini ya maendeleo katika elimu;
- f) stadi za uongozi na utawala katika elimu; na
- g) kumfundisha mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu.

1.6 Madhumuni ya Mafunzo ya Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu

Mwishoni mwa mafunzo ya Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu ya muda wa miaka miwili, mwalimu tarajali aweze:

- a) kutafsiri mtaala wa elimu ya msingi na mihtasari yake katika masomo darasani;
- b) kuandaa na kutumia njia shirikishi katika ufundishaji/ujifunzaji kwa kuzingatia mahitaji ya mwanafunzi;
- c) kubuni, kuendeleza na kufaragua zana za ufundishaji na ujifunzaji katika elimu ya msingi kwa kuzingatia mahitaji ya mwanafunzi;
- d) kufanya tafiti tatu za kielimu ili kuwabaini, kuwaendeleza na kuwasaidia wanafunzi wenye mahitaji maalumu katika shule za msingi;
- e) kurithisha desturi, maadili na tabia zinazokubalika kwa wanafunzi wa shule za msingi;
- f) kuchagua, kupanga, kusimamia na kuongoza vipindi darasani katika shule za msingi;
- g) kufundisha kwa ufanisi masuala mtambuka; na
- h) kutunga na kusahihisha majaribio na mitihani inayoendana na mtaala wa elimu ya msingi kwa kuzingatia mahitaji ya mwanafunzi katika nyanja zote tatu za kujifunza.

1.7 Umahiri wa Jumla wa Mafunzo ya Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu

Umahiri mkuu wa mafunzo ya Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu umejikita katika kumwandaa mwalimu tarajali aweze:

- a) kumbaini mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu, kujenga misingi ya kukubalika kwa wenzake, kwa jamii na kumpatia afua stahiki;
- b) kutumia mazingira wezeshi ya ufundishaji na ujifunzaji kwa mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu;
- c) kutumia njia mbalimbali za mawasiliano na teknolojia saidizi kwa kuzingatia mahitaji maalumu ya mwanafunzi;
- d) kutumia mbinu mbalimbali katika kutambua vipaji walivyonyo wanafunzi wenye mahitaji maalumu na namna ya kuviendeleza;

- e) kufanya tafiti tatuza za kielimu ili kuwabaini na kuwasaidia wanafunzi wenye mahitaji maalumu katika shule za msingi;
- f) kutumia misingi na stadi za uongozi katika kuongoza taasisi mbalimbali za elimu;
- g) kutumia, kutunza na kukarabati vifaa saidizi vya wanafunzi wenye mahitaji maalumu;
- h) kutumia sanaa na michezo rekebifu katika kuibua na kuendeleza vipaji mbalimbali vya wanafunzi wenye mahitaji maalumu;
- i) kutumia misingi ya ufundishaji na ujifunzaji kufundishia masomo ya taaluma;
- j) kujenga umahiri wa masomo kwa mwalimu tarajali utakaomwezesha kuelewa masomo vema na hivyo kumfundisha mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu; na
- k) kushirikiana na familia za wanafunzi wenye mahitaji maalumu katika kuwajengea wanafunzi hao kujiamini, tabia ya kujifunza na kukuza vipaji walivyonyo.

1.8 Malengo ya Somo la Upimaji na Afua Stahiki

Muhtasari huu wa somo la Upimaji na Afua Stahiki umeandaliwa ili kumwezesha mkufunzi kumuandaa mwalimu tarajali kufikia malengo yafuatayo:

- a) kufanya upimaji wa kumtambua mwanafunzi mwenye ulemavu wa akili na mwanafunzi mwenye usonji na kumpatia afua stahiki;
- b) kutumia mbinu mbalimbali katika kutambua vipaji walivyonyo wanafunzi wenye ulemavu wa akili na wanafunzi wenye usonji;
- c) kushirikiana na wadau wa elimu katika kutoa huduma kwa wanafunzi wenye ulemavu wa akili na wanafunzi wenye usonji; na
- d) kuandaa hatua za mpito kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa akili na mwanafunzi mwenye usonji ili kuwezesha ustawi wake.

1.9 Upimaji na Tathmini

Muhtasari huu umependekeza mbinu mbalimbali za upimaji na tathmini kwa kuzingatia mahitaji ya mwalimu tarajali wakati wa mchakato wa ujifunzaji wa kozi ya ualimu. Upimaji tamati utafanywa na Baraza la Mitihani la Tanzania na utakuwa na alama 50. Upimaji endelevu utafanywa na mkufunzi wakati mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji unaendelea na utakuwa na alama 50. Upimaji huu unahusisha majaribio, kazimradi, kazi binafsi, mkoba wa kazi, kazi kwa vitendo na mtihani wa mwisho wa muhula. Uzito wa kila aina ya upimaji umeoneshwa katika jedwali lifuatalo:

Jedwali namba 1: Upimaji Endelevu na Upimaji Tamati

Vipengele	Njia za Upimaji	Mwaka				Idadi	Alama (%)
		Mwaka wa I		Mwaka wa II			
		Muhula wa I	Muhula wa II	Muhula wa I	Muhula wa II		
Taaluma	Majaribio	1	1	1	1	4	10
	Kazimradi	-	-	1	-	1	5
	Kazi binafsi	1	1	1	-	3	5
	Kazi kwa vitendo	1	1	1	-	3	5
	Mkoba wa kazi	1	-	1	-	2	5
	Mtihani wa mwisho wa muhula	1	1	1	-	3	20
Upimaji endelevu							50
Upimaji tamati: Mtihani wa Baraza la Mitihani la Tanzania					1	1	50
Jumla ya alama za upimaji endelevu na upimaji tamati							100

1.10 Muda wa Mafunzo

Muhtasari huu wa somo la Upimaji na Afua Stahiki kwa fani ya ulemavu wa akili na usonji umekusudiwa kukamilishwa kwa kipindi cha miaka miwili. Mtazamo wa somo hili ni kumjengea mwalimu tarajali misingi muhimu ya maarifa ya somo la Upimaji na Afua Stahiki itakayomwezesha kufundisha kikamilifu mwanafunzi mwenye ulemavu wa akili na mwanafunzi mwenye usonji kumudu ujifunzaji katika elimu ya msingi.

1.11 Maudhui ya Muhtasari wa Somo

Maudhui ya muhtasari yamepangwa katika jedwali yakihusisha umahiri mkuu, umahiri mahususi, shughuli za kutendwa na mwalimu tarajali, vigezo vya upimaji, viwango vya utendaji na idadi ya vipindi

1.11.1 Umahiri

Ni uwezo wa kufikiri na kutenda kwa ufanisi

1.11.2 Umahiri Mkuu

Ni uwezo wa kutenda jambo kwa usahihi na ufanisi unaokusudiwa kufikiwa na mwalimu tarajali baada ya kujifunza kwa muda fulani. Hujengwa na umahiri mahususi atakaojengewa mwalimu tarajali kwa kutenda shughuli mbalimbali

1.11.3 Umahiri Mahususi

Ni uwezo atakaojengewa mwalimu tarajali katika kutenda shughuli mbalimbali kwa muda maalumu

1.11.4 Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali

Ni vitendo ambavyo mwalimu tarajali anapaswa kuvifanya ili kufikia umahiri mahususi uliokusudiwa

1.11.5 Vigezo vya Upimaji

Ni viwango vya ufanisi wa utendaji wa mwalimu tarajali ili kufikia umahiri mahususi

1.11.6 Viwango vya Utendaji

Ni kiasi cha ufikiwaji wa vigezo vya kila shughuli anayotenda mwalimu tarajali

1.11.7 Idadi ya Vipindi:

Idadi ya vipindi ni makadirio ya muda utakaotumika katika kufundisha na kujifunza kwa kuzingatia uzito wa umahiri mahususi na shughuli za kutendwa na mwalimu tarajali. Makadirio haya ya muda, yamewekwa kwa mfumo wa vipindi ambapo kila kipindi ni dakika 60. Somo hili litafundishwa kwa vipindi vitatu kwa wiki. Hata hivyo mapendekezo haya ya idadi ya vipindi yanaweza kubadilika kulingana na mazingira ya kufundishia na kujifunzia.

2.0 Maudhui ya Muhtasari

2.1 Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi wa Somo

Jedwali namba 2: Umahiri wa Somo la Upimaji na Afua Stahiki kwa Mwalimu Tarajali wa Fani ya Ulemavu wa Akili na Usonji

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi
1.0 Kufanya upimaji kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa akili na mwanafunzi mwenye usonji	1.1 Kujenga dhana ya upimaji kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa akili na mwanafunzi mwenye usonji 1.2 Kutumia hatua za upimaji kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa akili na wanafunzi wenye usonji

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi
	1.3 Kubaini nyanja za upimaji kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa akili na mwanafunzi mwenye usonji
2.0 Kutumia vifaa na zana za upimaji kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa akili na mwanafunzi mwenye usonji	2.1 Kuchambua zana za upimaji kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa akili na mwanafunzi mwenye usonji 2.2 Kubaini vifaa vya upimaji ili kutekeleza mazingira ya upimaji
3.0 Kutumia stadi za upimaji kutoa afua stahiki kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa akili na mwanafunzi mwenye usonji	3.1 Kuchambua mahitaji na afua stahiki kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa akili na mwanafunzi mwenye usonji 3.2 Kushirikiana na wadau wa elimu katika kutoa huduma kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa akili na mwanafunzi mwenye usonji 3.3 Kutumia upimaji na afua stahiki kubaini vipaji na vipawa
4.0 Kuandaa hatua za mpito kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa akili na mwanafunzi mwenye usonji	4.1 Kujenga dhana ya hatua za mpito kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa akili na mwanafunzi mwenye usonji 4.2 Kubaini wadau wa hatua za mpito 4.3 Kuainisha afua stahiki za hatua za mpito 4.4 Kufafanua mbinu za kuanzisha kitengo kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa akili na mwanafunzi mwenye usonji

2.2 Maudhui ya Ufundishaji wa Somo

Jedwali namba 3: Maudhui ya Ufundishaji wa Somo la Upimaji na Afua Stahiki kwa Mwalimu Tarajali wa Fani ya Ulemavu wa Akili na Usonji

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi	Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali	Vigezo vya Upimaji	Upimaji wa Viwango vya Utendaji				Idadi ya Vipindi
				Utendaji Chini ya Wastani	Utendaji wa Wastani	Utendaji Mzuri	Utendaji Mzuri Sana	
1.0 Kufanya upimaji kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa akili na mwanafunzi mwenye usonji	1.1 Kujenga dhana ya upimaji kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa akili na mwanafunzi mwenye usonji	a) Kufafanua dhana ya upimaji kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa akili na mwanafunzi mwenye usonji	Dhana ya upimaji imefafanuliwa.	Anafafanua maana ya upimaji kwa muktadha wa uzoefu wake binafsi.	Anafafanua maana ya upimaji kwa muktadha wa taaluma.	Anafafanua maana ya upimaji kwa muktadha wa taaluma na kutoa mifano.	Anafafanua maana ya upimaji kwa muktadha wa taaluma, anatoa mifano na kuhusianisha na mazingira.	16
		b) Kuhusianisha dhana ya upimaji na uhalisia wa upimaji	Dhana ya upimaji imehusianishwa na uhalisia kwa kueleza maana, umuhimu na kutoa mifano.	Anaeleza maana ya upimaji na kuhusianisha na dhana ya upimaji.	Anaeleza maana ya upimaji na kuhusianisha uhalisia wa upimaji.	Anaeleza maana ya upimaji, sifa na umuhimu wa upimaji na kutoa mifano.	Anaeleza maana ya upimaji, sifa na umuhimu wa kuhusianisha na uhalisia wa upimaji na kutoa mifano.	

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi	Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali	Vigezo vya Upimaji	Upimaji wa Viwango vya Utendaji				Idadi ya Vipindi
				Utendaji Chini ya Wastani	Utendaji wa Wastani	Utendaji Mzuri	Utendaji Mzuri Sana	
		c) Kueleza changamoto za upimaji kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa akili na mwanafunzi mwenye usonji	Changamoto sita za upimaji zimeelezwa.	Anaeleza changamoto mbili za upimaji.	Anaeleza changamoto tatu za upimaji.	Anaeleza changamoto tano za upimaji na kutoa mifano.	Anaeleza changamoto sita za upimaji, kutoa mifano na kuwasaidia wenzake.	
	1.2 Kutumia hatua za upimaji kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa akili na mwanafunzi mwenye usonji	a) Kufafanua hatua za upimaji kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa akili na mwanafunzi mwenye usonji	Hatua tatu za upimaji zimefafanuliwa na kutoa mifano kwa kuzingatia mazingira halisi.	Anafafanua hatua moja ya upimaji kwa kuzingatia mazingira halisi.	Anafafanua hatua mbili za upimaji kwa kuzingatia mazingira halisi.	Anafafanua hatua tatu za upimaji kwa kuzingatia mazingira na kutoa mifano.	Anafafanua hatua tatu za upimaji na kutoa mifano kwa kuzingatia mazingira na kuwaelekeza wenzake.	16

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi	Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali	Vigezo vya Upimaji	Upimaji wa Viwango vya Utendaji				Idadi ya Vipindi
				Utendaji Chini ya Wastani	Utendaji wa Wastani	Utendaji Mzuri	Utendaji Mzuri Sana	
		b) Kubainisha umuhimu wa kufuata hatua za upimaji kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa akili na mwenye usonji	Sababu nne muhimu za kufuata hatua za upimaji zimebainishwa.	Anabainisha sababu moja ya umuhimu wa kufuata hatua za upimaji.	Anabainisha sababu mbili muhimu za kufuata hatua za upimaji.	Anabainisha sababu tatu muhimu za kufuata hatua za upimaji na kutoa mifano.	Anabainisha sababu nne muhimu za kufuata hatua za upimaji, anatoa mifano kwa kuhusianisha na mazingira na kuwaelekeza wenzake.	
		c) Kujenga uwezo wa kufanya upimaji kwa kuzingatia hatua za upimaji	Uwezo wa kufanya mazoezi ya upimaji kwa kuzingatia hatua na mtiririko wa stadi tano umejengwa.	Anajenga stadi za kufanya upimaji kwa hatua pasipo kuzingatia mtiririko.	Anajenga stadi tatu za kufanya mazoezi ya upimaji kwa hatua na kuzingatia mtiririko.	Anajenga stadi nne za kufanya mazoezi ya upimaji kwa hatua na kuzingatia mtiririko na kutoa mifano.	Anajenga stadi tano za kufanya mazoezi ya upimaji kwa hatua na kuzingatia mtiririko, kutoa mifano na kuwaelekeza wenzake.	

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi	Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali	Vigezo vya Upimaji	Upimaji wa Viwango vya Utendaji				Idadi ya Vipindi
				Utendaji Chini ya Wastani	Utendaji wa Wastani	Utendaji Mzuri	Utendaji Mzuri Sana	
		d) Kufafanua dhana ya uhifadhi wa kumbukumbu na matokeo ya upimaji	Dhana ya uhifadhi wa kumbukumbu imefafanuliwa.	Anafafanua maana ya uhifadhi wa kumbukumbu.	Anafafanua maana na aina za uhifadhi wa kumbukumbu.	Anafafanua maana, aina na umuhimu wa uhifadhi kumbukumbu na kutoa mifano yake.	Anafafanua maana, aina na umuhimu wa uhifadhi kumbukumbu, kutoa mifano na kuwasaidia wenzake.	
		e) Kufafanua njia za uhifadhi wa kumbukumbu na matokeo ya upimaji	Njia tano za uhifadhi wa kumbukumbu na matokeo ya upimaji zimefafanuliwa.	Anafafanua njia moja ya uhifadhi wa kumbukumbu na matokeo ya upimaji.	Anafafanua njia mbili za uhifadhi wa kumbukumbu na matokeo ya upimaji.	Anafafanua njia nne za uhifadhi wa kumbukumbu na matokeo ya upimaji na kutoa mifano.	Anafafanua njia tano za uhifadhi wa kumbukumbu na matokeo ya upimaji, kutoa mifano na kuwasaidia wengine.	

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi	Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali	Vigezo vya Upimaji	Upimaji wa Viwango vya Utendaji				Idadi ya Vipindi
				Utendaji Chini ya Wastani	Utendaji wa Wastani	Utendaji Mzuri	Utendaji Mzuri Sana	
	1.3 Kubaini nyanja za upimaji kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa akili na mwanafunzi mwenye usonji	a) Kuchambua nyanja za upimaji kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa akili na mwanafunzi mwenye usonji	Nyanja nane za upimaji zimechambuliwa.	Anachambua nyanja mbili za upimaji.	Anachambua nyanja nne za upimaji.	Anachambua nyanja sita za upimaji na kutoa mifano.	Anachambua nyanja nane za upimaji, kutoa mifano na kuwaelekeza wengine.	16
		b) Kubainisha vigezo vya nyanja ya upimaji kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa akili na mwanafunzi mwenye usonji	Vigezo vitatu vya nyanja za upimaji zimebainishwa.	Anabainisha kigezo kimoja bila mpangilio katika nyanja ya upimaji.	Anabainisha vigezo viwili vya nyanja ya upimaji.	Anabainisha vigezo vitatu vya nyanja ya upimaji kwa mpangilio na kutoa mifano.	Anabainisha vigezo vitatu vya nyanja ya upimaji kwa mpangilio, kutoa mifano na kuwaeleza wenzake.	

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi	Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali	Vigezo vya Upimaji	Upimaji wa Viwango vya Utendaji				Idadi ya Vipindi
				Utendaji Chini ya Wastani	Utendaji wa Wastani	Utendaji Mzuri	Utendaji Mzuri Sana	
		c) Kujenga uwezo wa kufanya mazoezi ya upimaji kwa kuzingatia nyanja nane za upimaji	Uwezo wa kufanya mazoezi ya upimaji kwa kuzingatia nyanja nane za upimaji umejengwa.	Anajenga uwezo wa kufanya mazoezi ya upimaji kwa kuzingatia nyanja mbili za upimaji.	Anajenga uwezo wa kufanya mazoezi ya upimaji kwa kuzingatia nyanja nne za upimaji.	Anajenga uwezo wa kufanya mazoezi ya upimaji kwa kuzingatia nyanja sita za upimaji kwa mtiririko na kutoa mifano.	Anajenga uwezo wa kufanya mazoezi ya upimaji kwa kuzingatia nyanja nane za upimaji, kutoa mifano halisi na kuwaeleza wenzake.	
2.0 Kutumia vifaa na zana za upimaji kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa akili na mwanafunzi mwenye usonji	2.1 Kuchambua zana za upimaji kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa akili na mwanafunzi mwenye usonji	a) Kufafanua matumizi ya zana za upimaji kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa akili na mwanafunzi mwenye usonji	Matumizi sita ya zana za upimaji yamefafanuliwa.	Anafafanua matumizi mawili ya zana za upimaji.	Anafafanua matumizi matatu ya zana za upimaji na kutoa mfano.	Anafafanua matumizi manne ya zana za upimaji na kutoa mifano mbalimbali.	Anafafanua matumizi sita ya zana za upimaji, anatoa mifano na kuwaelekeza wengine.	16

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi	Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali	Vigezo vya Upimaji	Upimaji wa Viwango vya Utendaji				Idadi ya Vipindi
				Utendaji Chini ya Wastani	Utendaji wa Wastani	Utendaji Mzuri	Utendaji Mzuri Sana	
		b) Kueleza namna ya kutumia zana za upimaji kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa akili na mwanafunzi mwenye usonji	Namna sita ya kutumia zana za upimaji zimeelezwa kwa kutoa mifano.	Anaeleza namna mbili za kutumia zana za upimaji.	Anaeleza namna tatu za kutumia zana za upimaji.	Anaeleza namna tano za kutumia zana za upimaji kwa kutoa mifano.	Anaeleza namna sita za kutumia zana za upimaji kwa kutoa mifano na kuwaelekeza wengine.	
	2.2 Kubaini vifaa vya upimaji ili kutekeleza mazingira ya upimaji	a) Kubainisha vifaa vya upimaji	Vifaa vya upimaji vimebainishwa.	Anataja vifaa vya upimaji.	Anaeleza vifaa vya upimaji.	Anaeleza vifaa vya upimaji na kutoa mifano.	Anaeleza vifaa vya upimaji, kutoa mifano na kuhusianisha na mazingira.	16

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi	Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali	Vigezo vya Upimaji	Upimaji wa Viwango vya Utendaji				Idadi ya Vipindi
				Utendaji Chini ya Wastani	Utendaji wa Wastani	Utendaji Mzuri	Utendaji Mzuri Sana	
		b) Kueleza namna ya kutumia vifaa vya upimaji kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa akili na mwanafunzi mwenye usonji	Namna sita za kutumia vifaa vya upimaji imeelezwa.	Anaeleza namna mbili za kutumia vifaa vya upimaji.	Anaeleza namna tatu za kutumia vifaa vya upimaji.	Anaeleza namna nne za kutumia vifaa vya upimaji na kutoa mifano.	Anaeleza namna sita za kutumia vifaa vya upimaji, kutoa mifano na kuwaelekeza wengine.	
3.0 Kutumia stadi za upimaji kutoa afua stahiki kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa akili na mwanafunzi mwenye usonji	3.1 Kuchambua mahitaji na afua stahiki kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa akili na mwanafunzi mwenye usonji	a) Kufafanua dhana ya afua stahiki kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa akili na mwanafunzi mwenye usonji	Dhana ya afua stahiki imefafanuliwa kwa kuzingatia maana, aina, na umuhimu wake kwa kutoa mifano.	Anafafanua maana ya afua stahiki.	Anafafanua maana na aina za afua stahiki.	Anafafanua maana, aina na umuhimu wa afua stahiki na kutoa mifano.	Anafafanua maana, aina na umuhimu wa afua stahiki kwa kutoa mifano na kuwasaidia wengine.	16

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi	Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali	Vigezo vya Upimaji	Upimaji wa Viwango vya Utendaji				Idadi ya Vipindi
				Utendaji Chini ya Wastani	Utendaji wa Wastani	Utendaji Mzuri	Utendaji Mzuri Sana	
		b) Kufaragua vifaa vinavyotumika kutoa afua stahiki	Vifaa sita vinavyotumika kutoa afua stahiki vimefaraguliwa.	Anafaragua vifaa viwili vinavyotumika kutoa afua stahiki.	Anafaragua vifaa vitatu vinavyotumika kutoa afua stahiki.	Anafaragua vifaa vinne vinavyotumika kutoa afua stahiki na kutoa mifano.	Anafaragua vifaa sita vinavyotumika kutoa afua stahiki, kutoa mifano na kuwasaidia wengine.	
		c) Kueleza namna ya kutumia taarifa ya upimaji katika kutoa afua stahiki	Namna nne za kutumia taarifa ya upimaji katika kutoa afua stahiki zimeelezwa kwa kutoa mifano.	Anaeleza namna moja ya kutumia taarifa ya upimaji katika kutoa afua stahiki.	Anaeleza namna mbili za kutumia taarifa ya upimaji katika kutoa afua stahiki.	Anaeleza namna tatu za kutumia taarifa ya upimaji katika kutoa afua stahiki na kutoa mifano.	Anaeleza namna nne za kutumia taarifa ya upimaji katika kutoa afua stahiki, kutoa mifano na kuwasaidia wengine.	

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi	Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali	Vigezo vya Upimaji	Upimaji wa Viwango vya Utendaji				Idadi ya Vipindi
				Utendaji Chini ya Wastani	Utendaji wa Wastani	Utendaji Mzuri	Utendaji Mzuri Sana	
		d) Kuandaa afua stahiki kwa kuzingatia uhitaji	Aina sita za afua stahiki zimeandaliwa kwa kuzingatia uhitaji.	Anaandaa aina mbili za afua stahiki kwa kuzingatia uhitaji.	Anaandaa aina tatu za afua stahiki kwa kuzingatia uhitaji.	Anaandaa aina tano za afua stahiki kwa kuzingatia uhitaji na kutoa mifano.	Anaandaa aina sita za afua stahiki kwa kuzingatia uhitaji, kutoa mifano na kuwasaidia wengine.	
	3.2 Kushirikiana na wadau wa elimu katika kutoa huduma kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa akili na mwanafunzi mwenye usonji	a) Kubaini wataalamu shiriki katika utoaji wa afua stahiki	Wataalamu shiriki sita katika utoaji wa afua stahiki wamebainishwa kwa kuzingatia mazingira ya upatikanaji wao.	Anabaini wataalamu wawili katika utoaji wa afua stahiki kwa kuzingatia mazingira ya upatikanaji wao.	Anabaini wataalamu watatu katika utoaji wa afua stahiki kwa kuzingatia mazingira ya upatikanaji wao.	Anabaini wataalamu wanne katika utoaji wa afua stahiki kwa kuzingatia mazingira ya upatikanaji wao.	Anabaini wataalamu sita katika utoaji wa afua stahiki kwa kuzingatia mazingira ya upatikanaji wao na kuwaelekeza wengine.	16

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi	Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali	Vigezo vya Upimaji	Upimaji wa Viwango vya Utendaji				Idadi ya Vipindi
				Utendaji Chini ya Wastani	Utendaji wa Wastani	Utendaji Mzuri	Utendaji Mzuri Sana	
		b) Kueleza majukumu ya wadau katika kutoa afua stahiki	Majukumu sita ya wadau katika kutoa afua stahiki yameelezwa.	Anaeleza majukumu mawili ya wadau katika kutoa afua stahiki.	Anaeleza majukumu matatu ya wadau katika kutoa afua stahiki.	Anaeleza majukumu manne ya wadau katika kutoa afua stahiki.	Anaeleza majukumu sita ya wadau katika kutoa afua stahiki na kuwaelekeza wengine.	
		c) Kuandaa mpango kazi unaopendekeza huduma stahiki	Mpango kazi unaopendekeza huduma stahiki sita umeandaliwa.	Anaandaa mpango kazi unaopendekeza huduma stahiki mbili.	Anaandaa mpango kazi unaopendekeza huduma stahiki tatu.	Anaandaa mpango kazi unaopendekeza huduma stahiki tano.	Anaandaa mpango kazi unaopendekeza huduma stahiki sita na kuwaelekeza wengine.	
		d) Kubainisha stadi za kuhifadhi kumbukumbu za afua stahiki	Stadi sita za kuhifadhi kumbukumbu za afua stahiki zimebainishwa kwa kuzingatia mazingira.	Anabainisha stadi mbili za kuhifadhi kumbukumbu za afua stahiki kwa kuzingatia mazingira.	Anabainisha stadi tatu za kuhifadhi kumbukumbu za afua stahiki kwa kuzingatia mazingira.	Anabainisha stadi nne za kuhifadhi kumbukumbu za afua stahiki kwa kuzingatia mazingira.	Anabainisha stadi sita za kuhifadhi kumbukumbu za afua stahiki kwa kuzingatia mazingira na kuwaelekeza wengine.	

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi	Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali	Vigezo vya Upimaji	Upimaji wa Viwango vya Utendaji				Idadi ya Vipindi
				Utendaji Chini ya Wastani	Utendaji wa Wastani	Utendaji Mzuri	Utendaji Mzuri Sana	
	3.3 Kutumia upimaji na afua stahiki kubaini vipaji na vipawa	a) Kueleza dhana ya mwanafunzi mwenye kipaji na kipawa	Dhana ya mwanafunzi mwenye kipaji na kipawa imeelezwa.	Anaeleza maana ya mwanafunzi mwenye kipaji na kipawa.	Anaeleza maana ya mwanafunzi mwenye kipaji na kipawa na tofauti zake.	Anaeleza maana ya mwanafunzi mwenye kipaji na kipawa, tofauti zake na kutoa mifano.	Anaeleza maana ya mwanafunzi mwenye kipaji na kipawa, tofauti zake, kutoa mifano na kuwaelekeza wengine.	16
		b) Kufafanua njia na mbinu za kubaini vipaji na vipawa	Njia na mbinu sita za kubaini vipaji na vipawa zimefafanuliwa.	Anafafanua njia na mbinu mbili za kubaini vipaji na vipawa.	Anafafanua njia na mbinu tatu za kubaini vipaji na vipawa.	Anafafanua njia na mbinu nne za kubaini vipaji na vipawa na kutoa mifano.	Anafafanua njia na mbinu sita za kubaini vipaji na vipawa, kutoa mifano na kuwaelekeza wengine.	

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi	Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali	Vigezo vya Upimaji	Upimaji wa Viwango vya Utendaji				Idadi ya Vipindi
				Utendaji Chini ya Wastani	Utendaji wa Wastani	Utendaji Mzuri	Utendaji Mzuri Sana	
		c) Kueleza namna ya kuibua, kukuza na kuendeleza vipaji na vipawa kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa akili na mwanafunzi mwenye usonji	Namna ya kuibua, kukuza na kuendeleza vipaji na vipawa imeelezwa.	Anaeleza namna ya kuibua vipaji na vipawa.	Anaeleza namna ya kuibua na kukuza vipaji na vipawa.	Anaeleza namna ya kuibua na kukuza vipaji na vipawa kwa kutoa mifano.	Anaeleza namna ya kuibua na kukuza vipaji na vipawa kwa kutoa mifano na kuwaelekeza wengine.	
		d) Kubainisha eneo stahiki kutokana na kipaji na kipawa cha mwanafunzi mwenye ulemavu wa akili na mwanafunzi mwenye usonji	Maeneo sita stahiki ya kipaji na kipawa yamebainishwa.	Anabainisha maeneo mawili stahiki ya kipaji na kipawa.	Anabainisha maeneo matatu stahiki ya kipaji na kipawa.	Anabainisha maeneo manne stahiki ya kipaji na kipawa na kutoa mifano.	Anabainisha maeneo sita stahiki ya kipaji na kipawa, kutoa mifano na kuwaelekeza wengine.	

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi	Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali	Vigezo vya Upimaji	Upimaji wa Viwango vya Utendaji				Idadi ya Vipindi
				Utendaji Chini ya Wastani	Utendaji wa Wastani	Utendaji Mzuri	Utendaji Mzuri Sana	
		e) Kubaini stadi za masomo stahiki atakayoendelea nayo mwanafunzi mwenye ulemavu wa akili na mwanafunzi mwenye usonji baada ya hatua/ darasa aliyofikia	Stadi sita za masomo stahiki atakayoendelea nayo mwanafunzi mwenye ulemavu wa akili na mwanafunzi mwenye usonji baada ya hatua/ darasa aliyofikia zimebainishwa.	Anabainisha stadi mbili za masomo stahiki atakayoendelea nayo mwanafunzi mwenye ulemavu wa akili na mwanafunzi mwenye usonji baada ya hatua/ darasa aliyofikia.	Anabainisha stadi tatu za masomo stahiki atakayoendelea nayo mwanafunzi mwenye ulemavu wa akili na mwanafunzi mwenye usonji baada ya hatua/ darasa aliyofikia.	Anabainisha stadi nne za masomo stahiki atakayoendelea nayo mwanafunzi mwenye ulemavu wa akili na mwanafunzi mwenye usonji baada ya hatua/ darasa aliyofikia.	Anabainisha stadi sita za masomo stahiki atakayoendelea nayo mwanafunzi mwenye ulemavu wa akili na mwanafunzi mwenye usonji baada ya hatua/ darasa aliyofikia na kuwaeleza wengine.	

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi	Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali	Vigezo vya Upimaji	Upimaji wa Viwango vya Utendaji				Idadi ya Vipindi
				Utendaji Chini ya Wastani	Utendaji wa Wastani	Utendaji Mzuri	Utendaji Mzuri Sana	
4.0 Kuandaa hatua za mpito kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa akili na mwanafunzi mwenye usonji	4.1 Kujenga dhana ya hatua za mpito kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa akili na mwanafunzi mwenye usonji	a) Kueleza maana ya hatua za mpito	Maana ya hatua za mpito imeelezwa kwa kutoa mfano.	Anaeleza maana ya hatua za mpito.	Anaeleza maana ya hatua za mpito na kutoa mifano miwili.	Anaeleza maana ya hatua za mpito na kutoa mifano mitatu.	Anaeleza maana ya hatua za mpito na kutoa mifano minne na kuwaeleza wengine.	16
		b) Kubainisha hatua za mpito	Hatua mbili za mpito zimebainishwa kwa kuzingatia mikakati na utaratibu wake.	Anataja hatua moja ya mpito.	Anataja hatua mbili za mpito.	Anabainisha hatua mbili za mpito na mikakati yake.	Anabainisha hatua mbili za mpito, mikakati yake, anaandaa utaratibu kuhusu hatua hizo na kuwaeleza wengine.	

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi	Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali	Vigezo vya Upimaji	Upimaji wa Viwango vya Utendaji				Idadi ya Vipindi
				Utendaji Chini ya Wastani	Utendaji wa Wastani	Utendaji Mzuri	Utendaji Mzuri Sana	
		c) Kuchambua sababu za umuhimu wa hatua za mpito	Sababu nne za umuhimu wa hatua za mpito zimechambuliwa kwa kuhusianishwa na mazingira.	Anachambua sababu mbili za umuhimu wa hatua za mpito.	Anachambua sababu tatu za umuhimu wa hatua za mpito.	Anachambua sababu nne za umuhimu wa hatua za mpito.	Anachambua sababu nne za umuhimu wa hatua za mpito na kuhusianisha na mazingira husika.	
		d) Kueleza sababu za umuhimu wa kumuandaa mwanafunzi na hatua za mpito	Sababu nne muhimu za kumuandaa mwanafunzi na hatua za mpito zimeelezwa kwa kuzingatia mazingira halisi.	Anaeleza sababu moja muhimu ya kumuandaa mwanafunzi na hatua za mpito.	Anaeleza sababu mbili muhimu za kumuandaa mwanafunzi na hatua za mpito.	Anaeleza sababu tatu muhimu za kumuandaa mwanafunzi na hatua za mpito kwa kuzingatia mazingira halisi.	Anaeleza sababu nne muhimu za kumuandaa mwanafunzi katika hatua za mpito kwa kuzingatia mazingira halisi.	

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi	Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali	Vigezo vya Upimaji	Upimaji wa Viwango vya Utendaji				Idadi ya Vipindi
				Utendaji Chini ya Wastani	Utendaji wa Wastani	Utendaji Mzuri	Utendaji Mzuri Sana	
4.2 Kubaini wadau wa hatua za mpito	a) Kubaini wadau wa hatua za mpito nyumbani	Wadau wanne wa hatua za mpito nyumbani wamebainishwa kwa kuzingatia majukumu yao.	Anabaini mdau mmoja wa hatua za mpito nyumbani.	Anabaini wadau wawili wa hatua za mpito nyumbani.	Anabaini wadau watatu wa hatua za mpito nyumbani.	Anabaini wadau wanne wa hatua za mpito nyumbani kwa kuzingatia majukumu yao.	16	
	b) Kubaini wadau wa hatua za mpito katika shule ya awali	Wadau wanne wa hatua za mpito katika shule ya awali wamebainishwa kwa kuzingatia majukumu yao.	Anabaini mdau mmoja wa hatua za mpito katika shule ya awali.	Anabaini wadau wawili wa hatua za mpito katika shule ya awali.	Anabaini wadau watatu wa hatua za mpito katika shule ya awali.	Anabaini wadau wanne wa hatua za mpito katika shule ya awali kwa kuelezea majukumu yao.		
	c) Kubaini wadau wa hatua za mpito kwenye kitengo	Wadau wanne wa hatua za mpito kwenye kitengo wamebainishwa kwa kuzingatia majukumu yao.	Anabaini mdau mmoja wa hatua za mpito kwenye kitengo.	Anabaini wadau wawili wa hatua za mpito kwenye kitengo.	Anabaini wadau watatu wa hatua za mpito kwenye kitengo.	Anabaini wadau wanne wa hatua za mpito kwenye kitengo kwa kuzingatia majukumu yao.		

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi	Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali	Vigezo vya Upimaji	Upimaji wa Viwango vya Utendaji				Idadi ya Vipindi
				Utendaji Chini ya Wastani	Utendaji wa Wastani	Utendaji Mzuri	Utendaji Mzuri Sana	
		d) Kubaini wadau wa hatua za mpito baada ya kukamilisha hatua za shuleni	Wadau wanne wa hatua za mpito baada ya kukamilisha hatua za shuleni wamebainishwa kwa kuzingatia majukumu yao.	Anabaini mdau mmoja wa hatua za mpito baada ya kukamilisha hatua za shuleni.	Anabaini wadau wawili wa hatua za mpito baada ya kukamilisha hatua za shuleni.	Anabaini wadau watatu wa hatua za mpito baada ya kukamilisha hatua za shuleni.	Anabaini wadau wanne wa hatua za mpito baada ya kukamilisha hatua za shuleni kwa kuzingatia majukumu yao.	
	4.3 Kuainisha afua stahiki za hatua za mpito	a) Kubaini afua stahiki za kitabia	Afua stahiki za kitabia zimebainishwa kwa mifano na kuhusianishwa na mazingira.	Anabainisha tabia zinazohitaji afua stahiki.	Anabainisha tabia na afua stahiki zake.	Anabainisha tabia, afua stahiki zake na kutoa mifano.	Anabainisha tabia, afua stahiki zake, kutoa mifano na kuhusianisha na mazingira.	16
		b) Kubaini afua stahiki za kijamii	Afua stahiki za kijamii zimebainishwa kwa mifano na kuhusianishwa na mazingira.	Anabainisha maeneo ya kijamii yanayohitaji afua stahiki.	Anabainisha maeneo ya kijamii na afua stahiki zake.	Anabainisha maeneo ya kijamii, afua stahiki zake na kutoa mifano.	Anabainisha maeneo ya kijamii, afua stahiki zake, kutoa mifano na kuhusianisha na mazingira.	

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi	Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali	Vigezo vya Upimaji	Upimaji wa Viwango vya Utendaji				Idadi ya Vipindi
				Utendaji Chini ya Wastani	Utendaji wa Wastani	Utendaji Mzuri	Utendaji Mzuri Sana	
		c) Kubaini afua stahiki za kimawasiliano	Afua stahiki za kimawasiliano zimebainishwa kwa mifano na kuhusianishwa na mazingira.	Anabainisha maeneo ya kimawasiliano yanayohitaji afua stahiki.	Anabainisha maeneo ya kimawasiliano na afua stahiki zake.	Anabainisha maeneo ya kimawasiliano, afua stahiki zake na kutoa mifano.	Anabainisha maeneo ya kimawasiliano, afua stahiki zake, kutoa mifano na kuhusianisha na mazingira.	
		d) Kubaini afua stahiki za kitaaluma	Afua stahiki za kitaaluma zimebainishwa kwa mifano na kuhusianishwa na mazingira.	Anabainisha maeneo ya kitaaluma yanayohitaji afua stahiki.	Anabainisha maeneo ya kitaaluma na afua stahiki zake.	Anabainisha maeneo ya kitaaluma, afua stahiki zake na kutoa mifano.	Anabainisha maeneo ya kitaaluma, afua stahiki zake, kutoa mifano na kuhusianisha na mazingira.	

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi	Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali	Vigezo vya Upimaji	Upimaji wa Viwango vya Utendaji				Idadi ya Vipindi
				Utendaji Chini ya Wastani	Utendaji wa Wastani	Utendaji Mzuri	Utendaji Mzuri Sana	
4.4 Kufafanua mbinu za kuanzisha kitengo kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa akili na mwanafunzi mwenye usonji	a) Kueleza dhana ya kitengo cha elimu maalumu kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa akili na mwanafunzi mwenye usonji	Dhana ya kitengo cha elimu maalumu kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa akili na mwanafunzi mwenye usonji imeelezwa.	Anaeleza maana ya kitengo cha elimu maalumu kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa akili na mwanafunzi mwenye usonji.	Anaeleza maana na sifa ya kitengo cha elimu maalumu kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa akili na mwanafunzi mwenye usonji.	Anaeleza maana, sifa na umuhimu wa kitengo cha elimu maalumu kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa akili na mwanafunzi mwenye usonji.	Anaeleza maana, sifa na umuhimu wa kitengo cha elimu maalumu kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa akili na mwanafunzi mwenye usonji kwa mifano.	16	
		b) Kubainisha aina za vitengo kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa akili na mwanafunzi mwenye usonji	Aina mbili za vitengo zimebainishwa kwa kuzingatia ulemavu wa akili na huduma stahiki zinazoambatana nazo.	Anabainisha aina moja ya kitengo.	Anabainisha aina mbili za vitengo.	Anabainisha aina moja ya kitengo na huduma stahiki inayoambatana nazo na kutoa mifano.		Anabainisha aina mbili za vitengo na huduma stahiki zinazoambatana nazo kwa kutoa mifano na kuelekeza wengine.

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi	Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali	Vigezo vya Upimaji	Upimaji wa Viwango vya Utendaji				Idadi ya Vipindi
				Utendaji Chini ya Wastani	Utendaji wa Wastani	Utendaji Mzuri	Utendaji Mzuri Sana	
		c) Kubainisha hatua za kuzingatia kufungua kitengo kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa akili na mwanafunzi mwenye usonji	Hatua za kuzingatia wakati wa kufungua kitengo zimebainishwa (kwa kuzingatia ngazi ya shule, kata, tarafa, wilaya, mkoa na Taifa).	Anabainisha hatua za kufungua kitengo ngazi ya shule.	Anabainisha hatua za kufungua kitengo ngazi ya shule, kata na tarafa.	Anabainisha hatua za kufungua kitengo ngazi ya shule, kata, tarafa na wilaya na kutoa mifano.	Anabainisha hatua za kufungua kitengo ngazi ya shule, kata, tarafa, wilaya, mkoa na Taifa, kutoa mifano na kuelekeza wengine.	

Orodha ya Machapisho

- Hannah, L. (2001). *Teaching young children with autistic spectrum disorders to learn. A practical guide for parents and staff in mainstream schools and nurseries*. London, United Kingdoms: National Autistic Society.
- Heward, L. M. (2013). *Exceptional children; An introduction to special needs education*. Ohio, United States of America: Pearson.
- Inclusive Development Promoters & Consultants. (2016). *Kamusi elekezi ya ulemavu, kiingereza-kiswahili*. Dar es Salaam, Tanzania: Nesmap Printing Technology.
- Kaufman, A. S. (1994). *Intelligent testing with WISSC-III*. New York, United States of America: John Wiley & Sons.
- Overton, T. (2012). *Assessing learners with special needs, an applied approach, (7th ed.)*. Texa-Brownville, United States of America: Pearson.
- The National Academy of Sciences. (2001). *Knowing what the students know; The science and design of educational assessment. Committee on the Foundations of Assessment*: Washington DC, United States of America: National Academies Press.